



“ kwa nini tusilipe fadhila sisi kama Itilima kwa Mhe. Ras wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Jonh Magufuli Kwa kukusanya mapato vizuri, kwani Wilaya ya Itilima ndiyo Mnufaika namba moja wa fedha za kutoka serikali kuu Kimkoa” Mhe. Benson Kilangi

KIPAUMBELE NAMBA MOJA CHA SERIKALI NI MAKUSANYO YA MAPATO : DC ITILIMA



Mkuu wa Wilaya ya Itilima Mhe Benson Kilangi aliye simama, wapili Kutoka Kushoto Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Itilima Mhe. Mahamudu Mabula na wakwanza kulia Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya (W) Itilima Ndg. Kelisa Wambura

Mkuu wa wilaya ya Itilima Mhe. Benson Kilangi awataka viongozi Wilayani Itilima kufahamu yakuwa kipaumbele namba moja katika Bajeti ya mwaka 2019/2020 ni kuboresha ukusanyaji wa mapato.

Akitoa taarifa za Serikali katika Mkutano wa pili wa Baraza la Madiwani kwa mwaka 2018/2019 uliyofanyika katika ukumbi wa Nyalamu Mhe. Kilangi alisema

“ sisi viongozi tunaokaa na Makundi mbali mbali katika jamii ni lazima tumsaidie Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Mgufuli kutimiza malengo yake ya kutaka Tanzania ijitegemee Kiuchumi na katika hili lazima tuwaeleze watu ukweli kwamba watakiwa kulipa Kodi”

Aidha Mhe. Kilangi aliwataka viongozi na wananchi kwa ujumla kufahamu ya kwamba Maendeleo ya Kenya yenye idadi ya watu milioni 49.7 kwa takwimu za mwaka 2017, hayakuja bure, bali nikutokana na kuwa na idadi kubwa ya walipa kodi ambao ni takribani Milioni (8) nane, wakati Nchi yetu Tanzania yenye idadi ya watu takribani milioni 57.31 kwamujibu wa takwimu za mwaka 2017 ina idadi ya walipa kodi milioni (2)

“ kwa takwimu hizi unawezaje kupeleka huduma za maendeleo katika jamii ya watu karibu milioni 60 yenye walipa kodi milioni mbili tu, jibu ni haiwezekani” alisema Mhe. Kilangi.

Aidha Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Itilima aliwataka viongozi kumuelewa Rais Magufuli, anachokitaka ni kutengeneza walipakodi wengi Zaidi. Hata hivyo Mhe. Kilangi alitanabaisha ya kuwa Wilaya ya Itilima ndiyo mnufaika namba moja wa fedha za Serikali Kimkoa

“ katika hili lazima tuonyeshe shukrani kwa Serikali kwa kukusanya Mapato”

Mhe. Kilangi alisisitiza kuwa kama Wilaya tunakazi nyingi sana za kufanya, Ikiwemo Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na kuzitaka Kamati zote zinazo husika na ujenzi huo kujituma. Kuhusiana na ujenzi wa Madarasa kwa Mujibu wa Afisa Elimu Sekondali Mwl. Mtobi E. Kasembe alisema kuwa wanafunzi waliobaki nyumbani ni 109 lakini utaratibu wa kuwaomba

vikibali kwa Mkurugenzi cha kuanza masomo katika maboma ambayo hayajakamilika umeshafanyika.

Vile vile Mhe. Benson Kilangi alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri (W) Itilima Bi Elizabeth Gumbo na Mweka Hazina Ndg. Nuhu T. Moli kuwasaidia wanaochangisha fedha za jenzi wa madarasa, wachangishe katika mazingira yanayofaa

“ Kunamahali tumekuta pesa zinakusanywa na wachangiaji kuorodheshwa kwenye daftari, fedha za Umma zinatakiwa zikusanywe kwa utaratibu unaofaa ili baadaye zikagulike ikiwemo utolewaji wa stakabadhi kwa anaye changia” alisema Mhe. Kilangi.

Aidha, Mhe. Kilangi alitanabahisha Ujio wa Kamati ya Kamanda Siro wilayani Itilima na kuomba wapatiwe Ushirikiano kwani ujiowao ni kwa lengo la kuwabaini wapiga Lamli chonganishi.

Mhe. Mkuu wa Wilaya alimalizia kwa kuipongeza kamati ya Uratibu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa kazi nzuri iliyofanyika Mwaka uliyopita na kupelekea Itilima Kuongoza Kimkoa, kushika nafasi ya nne kikanda na kushika nafasi ya 22 kitaifa kati ya halmshauri Zaidi ya 180. Na kusisitiza Mshikamano uendeleo vilevile na kwa mwaha huu wa 2019/2020.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima Bi. Elizabeth Gumbo akitoa taarifa za Ofisi ya Mkurugenzi katika Mkutano wa pili wa Baraza la Madiwani kwa mwaka 2018/2019, katikati ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itilima Mhe. Daudi Nyalamu, wa mwisho ni Makamo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itilima Mhe Salum Lugundiga.